**KAULI YA SERIKALI KUHUSU HALI YA CHAKULA NA LISHE NCHINI MWAKA 2016/17 ILIYOTOLEWA NA MHE. ENG. DKT CHARLES JOHN TIZEBA (MB) WAZIRI WA KILIMO MIFUGO NA UVUVI TAREHE JANUARI 31, 2017**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kanuni namba 49, naomba kutoa Kauli ya Serikali kuhusu Hali ya Chakula na Lishe kwa mwaka 2016/2017.

**Mheshimiwa Spika,** utakumbuka katika Bunge lako la 10, Serikali ilitoa Kauli yake kuhusu upatikanaji na mahitaji ya chakula baada ya kukamilisha tathimini ya awali ya uzalishaji wa mazao ya chakula kwa mwaka 2015/16 na upatikanaji wa chakula mwaka 2016/2017. Katika Kauli hiyo ya Serikali, Bunge lako lilielezwa kuwa Tathimini, ilionyesha kuwa kitaifa, uzalishaji wa chakula utafikia tani **16,172,841** za chakula na mahitaji ya chakula kwa mwaka 2016/17 ni tani **13,159,326**, na hivyo nchi kuwa na ziada ya chakula tani **3,013,515.** Kati ya ziada hiyo, tani **1,101,341** ni za mazao ya nafaka na tani **1,912,174** ni za mazao yasiyo nafaka. Nchi ilikuwa na kiwango cha utoshelevu wa kiwango cha **asilimia 123.** Aidha, pamoja na hali nzuri ya chakula kitaifa, kulikuwa na **Halmashauri**

**43** ambazo zilikuwa na maeneo yenye upungufu wa chakula.

**Mheshimiwa Spika,** mwezi Januari 2017, Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine wa masuala ya Usalama wa Chakula na Lishe imekamilisha tathmini ya kina ya hali ya chakula na lishe nchini zikiwemo Halmashauri 43 zilizobainishwa awali kuwa na upungufu wa chakula. Tathmini hii ilishirikisha Shirika la Umoja wa Mataifa la Kilimo na Chakula (FAO) na Mpango wa Chakula Duniani (WFP). Aidha, Wataalamu kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) na Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) na Wizara ya Afya kupitia Tasisi yake ya Chakula na Lishe (TFNC) walishiriki. Tathimini hii imebainisha kuwa kuna Halmashauri 55 zenye upungufu wa chakula.

**Mheshimiwa Spika**, lengo kuu la Tathmini lilikuwa ni kuainisha mwenendo wa uzalishaji wa mazao ya chakula, na masuala yanayohusiana na lishe katika msimu wa 2015/2016 na athari zake katika mifumo ya maisha ya wananchi katika maeneo husika kwa kipindi cha Januari 2017 na matarajio kwa kipindi cha Mei 2017 kabla ya mavuno ya msimu wa 2016/2017. Matokeo ya Tathmini ya kina yameiwezesha Serikali kuchukua maamuzi stahiki katika utekelezaji wa jukumu la hali endelevu ya usalama wa chakula na lishe nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Tathimini hii ilizingatia mihimili minne ya usalama wa chakula ambayo ni **Upatikanaji wa chakula** (*Food availability*), **Ufikiwaji wa chakula** (*Food accessibility*), **Utumiaji wa chakula** (*Food utilization*) na **Uthabiti wa chakula** (*Food* s*tability)*. Aidha, ilitumia Mfumo wa Uanishaji wa Madaraja mbalimbali ya Usalama wa Chakula na Lishe - *Intergrated Food Security Phase Classification* (IPC) unaotumika kimataifa katika kuainisha watu na hali mbalimbali za makundi (*phases*) kiusalama wa chakula na lishe na aina ya hatua stahiki za kukabiliana nazo. Mfumo huu umewezesha kuchanganua vigezo mbalimbali na kutoa taswira ya hali halisi ilivyo kuanzia Julai, 2016 hadi Januari, 2017 na hali inavyotarajiwa katika kipindi kijacho kuanzia mwezi Februari hadi Mei 2017.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya hali ya upatikanaji wa mvua kutoka mikoa inayopata mvua za vuli, zinaonyesha kuwa kwa ujumla mvua zimechelewa kuanza na zimenyesha katika kiwango cha wastani na chini ya wastani zikiwa na mtawanyiko usioridhisha. Mikoa ya Kagera, Mwanza, Geita, Mara, Pwani, Tanga, Morogoro pamoja na sehemu ya mkoa wa Shinyanga na Simiyu mvua zilipoanza kunyesha zilikuwa chini ya wastani. Ukosefu wa mvua za vuli uliipata pia mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara. Mazao yaliyopandwa katika baadhi ya maeneo hayo yameathirika kutokana na ukame

uliojitokeza ukiwamo mkoa wa Kagera wilaya za Kyerwa, Missenyi na Karagwe.

**Mheshimiwa Spika,** kipindi cha mvua za Msimu kilichoanza mwezi Novemba, 2016 kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka - *Unimodal* (Mikoa ya Kigoma Tabora, Katavi, Singida Dodoma, Rukwa, Songwe, Mbeya, Iringa, Njombe, Ruvuma, Lindi na Mtwara) zinatarajiwa kuendelea hadi Aprili, 2017. Kwa ujumla mvua hizi zinatarajiwa kuwa za wastani katika maeneo mengi isipokuwa maeneo ya kaskazini mwa mkoa wa Lindi yanatarajiwa kupata mvua chini ya wastani katika kipindi cha mwezi Januari hadi Februari, 2017.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imekuwa na inaendelea kufuatilia mwenendo wa bei za mazao ya chakula hususan Mahindi, Mchele na Maharage ili kujiridhisha uwepo na upatikanaji wake sokoni. Bei ya wastani ya mahindi katika msimu wa chakula na soko kwa mwaka 2016/2017 imekuwa na mwelekeo wa kupanda kuanzia mwanzo wa mwezi Julai, 2016. Bei hii iko juu ikilinganishwa na bei katika kipindi kama hicho mwaka 2015. Hadi tarehe 23 Januari 2017, bei ya mahindi kwa gunia la kilo 100 imepanda na kufikia wastani wa kitaifa wa **shilingi 92,057.00** ikilinganishwa na Januari 2016 ambapo gunia la kilo 100 liliuzwa kwa wastani wa **shilingi 67,048.00.**

Kwa upande wa mchele bei zina mwelekeo mzuri bado kwa ulinganisho na mwaka jana, bado haijabadilika sana.

**Mheshimiwa Spika**, kupanda na kushuka kwa bei kwa kipindi kama hiki ni jambo lililotegemewa kwani mwanzo wa msimu hakuna mazao yanayoingia sokoni na hivyo hupelekea bei kupanda. Aidha, mwanzo wa mavuno bei hushuka kutokana na mazao mengi kuingia sokoni.. Hali ya mwenendo usioridhisha wa unyeshaji wa mvua za vuli na za msimu kwa kipindi cha 2016/17 kwa ajili ya upatikanaji wa chakula kwa mwaka 2017/18 katika maeneo mengi ya nchi, imechangia wafanyabiashara wa nafaka nchini na hasa zao la mahindi kuingiza zao hili kidogo kidogo sokoni, hivyo kuongeza kasi ya uhitaji kutoka kwa wananchi na kusababisha bei kuzidi kupanda. Aidha, uwepo wa mahitaji makubwa na bei nzuri ya mahindi katika nchi jirani zinazotuzunguka ambazo zilikuwa na upungufu wa chakula kumesababisha bei ya mahindi kuzidi kupanda.

**Mheshimiwa Spika,** tathmini ya kina ya hali ya chakula na lishe imekamilishwa. Matokeo ya tathmini hii yamebainisha kuwa hali ya upatikanaji wa chakula bado ni ya kuridhisha pamoja na kuwa na maeneo yenye upungufu wa chakula hapa nchini. Tathmini imebainisha kuwa **jumla ya tani 35,491 za chakula** zinahitajika ili

kukabiliana na hali ya upungufu wa chakula na lishe kati ya mwezi Februari na Aprili 2017 kwa **watu 1,186,028** walioainishwa kuwa wana upungufu wa chakula katika **Halmashauri 55.** Aidha, jumla ya **watu 118,603** wasio na uwezo wa kupata chakula (*destitute population*) watahitaji **tani 3,549** za chakula cha bei nafuu haraka. Serikali, imekwishaanza kuchukua hatua kukabiliana na hali hiyo ikiwamo ya kuuza chakula kwa bei nafuu katika maeneo yaliyobainishwa kuwa na upungufu mkubwa ili kushusha bei iliyopo na hatimaye kuwawezesha wananchi wa kipato cha chini kumudu bei.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na kuchelewa kwa mvua na mtawanyiko usioridhisha katika maeneo mengi hapa nchini, athari zifuatazo zinatarajiwa kutokea:-

i) Matarajio ya malengo ya uzalishaji wa mazao ya chakula huenda yasifikiwe,

ii) Uzalishaji wa mbegu za mazao ya kilimo utapungua,

iii) Uwezekano wa kuongezeka kwa bei za baadhi ya mazao ya chakula,

iv) Kupungua kwa mapato yatokanayo na ushuru wa mazao kwa baadhi ya Halmashauri,

v) Uwezekano wa kuwa na maeneo mengi yenye upungufu wa chakula na hivyo kuongezeka kwa kiwango cha utapiamlo,

vi) Kuongezeka kwa migogoro kati ya wakulima na wafugaji kutokana na uhaba wa malisho na maji,

vii) Uwezekano wa kupungua kwa mapato yatokanayo na mazao ya kilimo yanayouzwa nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** Ili kukabiliana na athari za ukame kama nilivyozieleza hapo juu, tathmini imebanisha kuwa Halmashauri za **wilaya 55** zinahitaji jumla ya **tani 1,969** za mbegu bora za mahindi, mtama na mizizi inayokomaa kwa muda mfupi na kustahimili ukame. Mbegu hizo zinahitajika ziwafikie mwezi Februari 2017 ili ziweze kupandwa katika msimu wa 2016/2017 katika maeneo yanayoendelea kupata mvua wakati huu wa mwaka.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali sasa inachukua hatua za makusudi kuhakikisha kuwa hali ya chakula na lishe ni imara na hatua hizi ni pamoja na:-

i) Kusimamia usambazaji wa mbegu za mazao ya kilimo zinazostahimili ukame na zinazozaa kwa muda mfupi ambazo ni pamoja na mtama, uwele na mbegu za mazao aina ya mizizi za mihogo na viazi vitamu ili kuzitumia vizuri mvua zinazonyesha sasa. Wizara

ilikutana na Wazalishaji wa mbegu za mazao ya kilimo Jijini Arusha mnamo Oktoba, 2016 ili kubaini mahitaji ya mbegu ikiwa ni pamoja na usambazaji wa mbegu hizo ili ziweze kuwafikia wakulima kwa wakati.

ii) Kuhamasisha wakulima kupanda mazao aina ya mizizi, mtama na uwele kwa maeneo yanayopata mvua za masika ambazo zinaendelea kunyesha na Mawakala wa pembejeo pamoja na vituo vya utafiti vilivyopo katika kanda mbalimbali hapa nchini.

iii) Serikali kupitia Wakala (NFRA) itaendelea kuhifadhi kwa uangalifu chakula kilichopo ili kitumike pale kitakapohitajika

iv) Kuhamasisha sekta binafsi kununua mazao ya chakula katika maeneo yaliyo na ziada bado na kuyauza katika maeneo yenye uhaba wa chakula. Aidha, wafanyabiashara waliohifadhi mahindi wanaombwa kusambaza chakula hicho katika masoko ya ndani ya nchi jambo ambalo litasaidia kupunguza mfumuko wa bei.

v) Kuhimiza usindikaji wa mazao ya chakula kwa kuyaongezea thamani na kuwaelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kula vyakula vya aina zote.

vi) Kutokana na hali ya mwenendo wa unyeshaji wa mvua za vuli na msimu kutokuridhisha katika maeneo mengi

ya nchi, Wakuu wa Mikoa na Wilaya wanashauriwa kuendelea kuhamasisha na kusimamia wakulima kutumia mbegu zinazokomaa mapema na kupanda mazao yanayostahimili ukame.

vii) Kuwashauri Wananchi kutumia kwa uangalifu, kutunza na kuhifadhi akiba ya chakula kwa matumizi ya kaya.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo napenda kusisitiza kuwa Serikali itaendelea kufuatilia hali ya chakula na lishe nchini kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ili kuhakikisha kuwa hali ya chakula na lishe hapa nchini ni imara wakati wote. Aidha, wakulima waendelee kuzitumia mvua zinazoendelea kunyesha kwa kupanda mazao yanayostahimili ukame na kukomaa kwa muda mfupi na pia waendelee kutunza na kutumia chakula walichonacho kwa uangalifu.

**Mheshimiwa Spika**, nakushukuru wewe na Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha.

**Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi** **Dodoma, 2017**